# AckySHINE.com

# Sababu za ukeketaji

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Hakuna hata mmoja anayejua hasa kwa nini, na lini desturi imeanza. Jamii inatoa maelezo tofauti kwa nini wasichana wanatakiwa watahiriwe. Sababu zifuatazo zimetolewa kufanya desturi hii: mila na utamaduni, dini, usafi, kulinda ubikira, kukaa bila kuzini. Kila mara sababu zinazotolewa za kuondoa au kukata kisimi ni kupunguza nyege au starehe kwa mwanamke. Kwa makosa, baadhi ya watu huamini kuwa kwa njia hii wanawake watakuwa waaminifu kwa waume zao. Kiafya hakuna sababu ya kumtahiri msichana, kinyume chake inaweza kusababisha idadi ya matatizo ya afya. Ukeketaji hautakiwi na dini yoyote. Hatakiwi na Koran wala Biblia. Ukeketaji ni desturi na mila ambayo imepitishwa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.